*Namba ya Mtahiniwa ………………………………………………*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA TANGANYIKA**
**MTIHANI WA UTAMILIFU KIDATO CHA NNE**

# KISWAHILI

**021**
**Muda: Saa 3:00** **Aprili, 2023**

**MAELEKEZO**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, na C zenye jumla ya maswali kumi na moja (11).
2. Jibu maswali yote kutoka Sehemu A na B na maswali mawili kutoka Sehemu C. Swali la 11 ni la lazima.
3. Sehemu A ina alama 16, Sehemu B alama 54 na Sehemu C alama 30.
4. Zingatia maelekezo ya kila sehemu na kila swali.
5. Vitu visivyoruhusiwa katika vyumba vya mtihani kamwe visiingie.
6. Andika namba ya upimaji katika kila ukurasa.

**KWA AJILI YA WASAHIHISHAJI TU**

| NAMBARI YA SWALI | ALAMA | SAINI YA MSAHIHISHAJI |
|---|---|---|
| 01 | | |
| 02 | | |
| 03 | | |
| 04 | | |
| 05 | | |
| 06 | | |
| 07 | | |
| 08 | | |
| 09 | | |
| 10 | | |
| 11 | | |
| **JUMLA** | | |
| **SAINI YA MHAKIKI** | | |

**SEHEMU A (ALAMA 16)**

Jibu maswali yote katika Sehemu hii.

1. Chagua herufi ya jibu sahihi katika vipengele (i) hadi (x) kisha andika herufi ya jibu sahihi katika karatasi yako ya kujibia.

(i) Bainisha tabia ya umbo lililopigiwa mstari katika kitenzi "ibwa."
A. Kauli ya kutendeka
B. Kauli ya kutendea
C. Kauli ya kutendeana
D. Kauli ya kutendwa
E. Kauli ya kutendewa

(ii) Bainisha jozi sahihi ya vipera vya Sanaa za Maonesho:
A. Muziki, fasihi, ususi, uhunzi na utarizi
B. Tarihi, ngano, visasili, soga na hadithi.
C. Ngonjera, miviga, ngoma, tambiko na majigambo
D. Maigizo, viechekesho, majigambo, lakabu na maghani
E. Michezo ya watoto, utani, ngonjera, mizungu na muziki

(iii) Neon "beberu" limeundwa kwa njia ipi kati ya hizi zifuatazo za uundaji wa maneno?
A. Kutumia fasili sisisi
B. Kuangalia athari za kitu
C. Kuhamisha maana ya neno
D. Kuangalia kazi ya kitu
E. Kuangalia sauti, sura na tabia

(iv) "Mtangazaji wa televisheni huhakikisha watazamaji wanapata habari sahihi kwa wakati." Katika fasihi, kazi hiyo hufanywa na nani kati ya hawa wafuatao?
A. Wasikilizaji
B. Hadhira
C. Fanani
D. Wasomaji
E. Wazungumzaji

(v) Mende anapenda uchafu. Neno lililopigiwa mstari lipo katika ngeli ipi?
A. KI – VI
B. U – I
C. A – WA/YU – A – WA
D. KU
E. LI – YA

(vi) Mofimu –me- katika sentensi "Rosa amenitaarifu leo asubuhi" ni:
A. Kiambishi awali kikanushi
B. Kiambishi awali cha njeo
C. Kiambishi awali cha urejeshi

D. Kiambishi awali cha nafsi ya tatu
E. Kiambishi tamati cha kutendesha

(vii) Mzee Jimbi na Kifaruhande ni miongoni mwa wahusika katika Tamthiliya ya ______.
A. Kilio Chetu
B. Takadini
C. Orodha
D. Ngoswa – Penzi Kitovu cha Uzembe
E. Joka la Mdimu

(viii) Ashirafu na Hamisi wakati wanaandika barua rasmi walisahau kujumuisha hatua inayofuata baada ya kipengele cha mwisho wa barua. Ni hatua ipi iliyokuwa imesahaulika ?
A. Jina la Mwandishi
B. Cheo cha Mwandishi
C. Salamu za maagano
D. Saini ya Mwandishi
E. Anuani ya Mwandikiwa

(ix) Tamathali ya semi inayotumika kufananisha vitu bila kiunganishi huitwa _________.
A. Tashibiha
B. Tashihisi
C. Sitiari
D. Tashititi
E. Taniaba

(x) "Kutwa mara tatu”. Dhima ya muundo wa mazungumzo haya ni ipi?
A. Kupunguza ukali wa mazungumzo
B. Kufupisha urefu wa mazungumzo
C. Kupamba lugha ya mazungumzo
D. Kuonesha msisitizo
E. Kukidhi haja ya mazungumzo

2. Oanisha maana za tamathali za semi zilizopo katika **Orodha A** na tamathali husika kutoka **Orodha B**, kisha andika herufi ya jibu sahihi katika kijitabu chako cha kujibia.

| ORODHA A | ORODHA B |
|---|---|
| (i) Ushangaaji wa jambo fulani, aghalabu huambatana na alama ya mshangao.<br>(ii) Upangiliaji wa maneno katika namna ya kupingana ili kusisitiza mawazo fulani.<br>(iii) Ulinganishaji wa vitu viwili au zaidi vyenye sifa tofauti kwa | A. Tashbiha<br>B. Takriri<br>C. Sitiari<br>D. Tabaini<br>E. Tashihisi<br>F. Nidaa<br>G. Tashititi<br>H. Tanakalisauti |

| | |
|---|---|
| kutumia viunganishi.<br>(iv) Uhuishwaji w akitu kisichobinadamu kupewa uwezo wa kutenda kama binadamu.<br>(v) Urudiaji wa meneno ili kuonesha msisitizo wa jambo.<br>(vi) Huuliza swali hali jibu linafahamika wazi. | I. Balagha |

**SEHEMU B (ALAMA 54)**

Jibu maswali yote kutoka sehemu hii

3. Kwa kutumia mifano, taja vipashio sita vya kiima.

4. Kwa kutumia hoja tatu (3), eleza faida za kutumia lugha fasaha na hoja tatu (3) hasara za kutumia lugha isiyo fasaha.

5. Andika rejesta tatu (3) zinazotumika katika miktadha ifuatayo:
   (a) Bungeni
   (b) Michezoni
   (c) Shuleni
   (d) Mtaani
   (e) Kwenye nyumba za ibada
   (f) Gulioni/mnadani

6. (a) Eleza kirefu cha neno BAKITA.
   (b) Eleza kazi nne (4) za BAKITA.

7. Kwa kutumia mifano kuntu kutoka katika tamthiliya ya Kilio Chetu na Orodha, eleza kwa kifupi namna Mwanamke alivyochorwa katika sura tofauti tofauti. (Hoja tatu (3) kutoka kila tamthiliya.)

8. Soma shairi lifuatalo kisha jibu maswali yanayofuata:

   1. Enyi vijana sikiliza, nawapa wangu wosia,
      Nataka kuwaeleza, ushauri ulo mwema,
      Hakika nawapongeza, hapa mlipofikia,
      Hongereni, hongereni, Hongereni kuhitimu.

   2. Ni mbali mlipofikia, kamwe msijebweteka,
      Matashi yenu kufikia, huo ni mwanzo sikia,
      Usije kuvitupia, vitabuvyo kwenye taka,
      Hongereni, hongereni, Hongereni kuhitimu.

   3. Shuleni mmejifunza, kusoma kwa uhakika,
      Kwa umakini mkajifunza, Kiswahili bila kuchoka,

Lugha mkajifunza, bila hata kubweteka,
Hongereni, hongereni, Hongereni kuhitimu.

**MASWALI**

(a) Andika kichwa cha shairi hili kwa maneno yasiyozidi manne.
(b) Neno "bweteka" lina maana gani kadiri ya lilivyotumika katika shairi hili?
(c) Mwandishi ametumia muundo gani?
(d) Taja tamathali mojawapo ya semi iliyotumika katika beti zote za shairi na mfano wa tamathali hiyo.
(e) Taja idadi ya mizani zilizopo katika mstari wa kwanza wa ubeti wa pili.

**SEHEMU C (ALAMA 30)**

Jibu maswali **mawili** (2) kutoka sehemu hii. Swali la 11 ni la lazima.

9. Fasihi simulizi ni ndizi ambazo huweza kubebwa katika vifungashio vya rangi tofauti. Eleza vifungashio vinne (4) na uelezee changamoto moja kwa kila kifungashio.

10. Mshairi hutumia taswira mbalimbali katika kufikisha ujumbe katika jamii. Dhihirisha dai hilo kwa kutumia diwani mbili ulizosoma. (Hoja tatu kwa kila diwani.)

11. Watanzania wa leo hawahitaji sio tu kiongozi bora bali mwenye uthubutu katika kupambania mahitaji yao. Kwa kutumia riwaya mbili ulizosoma, jadili mambo ambayo kiongozi anapaswa kuyakemea katika jamii.